

**HOTUBA YA MHESHIMIWA CHARLES MAKONGORO NYERERE
MKUU WA MKOA WA RUKWA WAKATI ALIPOFUNGUA KIKAO
CHA TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA MKATABA WA LISHE KWA
KIPINDI CHA JULAI, 2022 HADI JUNI, 2023 KILICHOFANYIKA
TAREHE 25 JULAI, 2023**

- ***Katibu Tawala Mkoa,***
- ***Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya,***
- ***Wakurugenzi wa Halmashauri,***
- ***Makatibu Tawala Wilaya,***
- ***Wakuu wa Seksheni na Vitengo Sekretarieti ya Mkoa,***
- ***Wakuu wa Idara wa Halmashauri,***
- ***Wadau wa Maendeleo (lishe endelevu),***
- ***Wajumbe wa Timu ya uendeshaji wa huduma za Afya
ya Mkoa na Halmashauri,***
- ***Waandishi wa Habari,***
- ***Mabibi na Mabwana.***

Awali ya yote napenda kutumia fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema ambaye ametuwezesha kuwa hapa leo tukiwa na afya njema. Kwa namna ya pekee nitoe shukrani za kipekee kwa wadau wetu wa maendeleo kutoka Mradi wa Lishe Endelevu kwa kuhudhuria katika kikao hiki muhimu, pia naomba nichukue nafasi hii kuwashukuru wote kwa kuitikia wito wa kikao hiki muhimu, **karibuni sana.**

Ndugu washiriki, Mkataba wa Lishe umekuwa ukitekelezwa nchini Tanzania kwa miaka sita (06) sasa tangu Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan alipoagiza kuwepo na Mkataba wa Usimamizi wa shughuli za Lishe kati yake na Wahe. Wakuu wa Mikoa yote 26 ya Tanzania Bara mwezi Agosti, 2017 Kutokana na hali ya lishe na udumavu kwa watoto chini ya miaka mitano nchini kuwa mbaya.

Ndugu washiriki, Ikumbukwe kuwa Mkataba umelenga katika kutekeleza Mpango Mkakati wa Lishe - ***National Multisectoral Nutrition Action Plan*** (NMNAP II) wa mwaka 2022/2026, Kwa kuwa shughuli za Lishe ni muhimu katika kukuza na kuendeleza jamii.

Ndugu washiriki, Leo tupo hapa kwa lengo la kutekeleza azimio hilo, hiki kikiwa ni Kikao chetu cha saba baada ya kufanya Kikao cha Sita cha tarehe 10 Februari, 2023. Katika Kikao hiki tutajadili kuhusu utekelezaji wa mkataba wa utendaji kazi na usimamizi wa shughuli za lishe katika Mkoa na Halmashauri zetu. Katika tathmini hii tutaangalia viashiria vya kadi alama ya lishe kwa kipindi cha Julai 2022 hadi Juni, 2023 ambavyo vitatuonyesha hali halisi ya utendaji wetu katika afua za lishe na kujadili kwa kina sababu za baadhi ya viashiria

kutotekelezwa kama ilivyotarajiwa na kuweka mikakati thabiti ya kuongeza kasi ya utekelezaji.

Ndugu washiriki, tunafahamu kwamba Mkoa wetu nao unapimwa utendaji kazi wake sawa na Mikoa mingine, hivyo katika kikao cha Tathmini ya Sita ya kitaifa iliyofanyika tarehe 30 Septemba, 2022 ilionesha kuwa, Mkoa wa Rukwa ulipata wastani wa asilimia **80** na kushika nafasi ya 1 Kitaifa kwa mwaka 2021/2022. Aidha kwa taarifa za kipindi cha Julai - Juni 2022/23 inaonesha kiashiria cha kutenga fedha na kutumia kwa mapato ya ndani kimepata rangi ya Kijani **(97.16)**.

Ndugu washiriki, Matarajio yangu ni kuwa katika kikao hiki tutajadili mambo ambayo yataongeza msukumo wa Usimamizi na Uelewa wa Masuala ya Lishe katika ngazi zote ili kupunguza kiwango cha Utapiamlo nchini kulingana na malengo ya mpango jumuishi wa Kitaifa wa lishe.

Ndugu washiriki, Naomba nimalizie kwa kuwataka mshiriki kikamilifu katika majadiliano kwa ustawi wa Lishe katika Mkoa wetu.

Kwa maneno hayo machache naomba kusema kuwa mkutano wetu wa siku moja wa kujadili utekelezaji wa mkataba wa

utendaji kazi na usimamizi wa shughuli za lishe kwa kipindi cha Julai 2022 - Juni 2023 kimefunguliwa.

**LISHE BORA KWA MAENDELEO YA UCHUMI WA
VIWANDA**

*Mungu Ibariki Tanzania,
Mungu Bariki Mkoa wetu wa Rukwa,*

Asanteni kwa Kunisikiliza

**Charles Makongoro Nyerere,
Mkuu wa Mkoa wa Rukwa.**